# Serikali Mtandao Kuboresha Utoaji Huduma kwa Umma

***Na Mambwana Jumbe***

Utekelezaji wa Serikali Mtandao ni moja ya sehemu muhimu ya maboresho yaliyofanyika katika Utumishi wa Umma, ambao umesaidia kurahisisha utoaji wa huduma zinazopatikana kwa urahisi na kwa gharama nafuu kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Utekelezaji wa Serikali Mtandao umejikita katika kuboresha utoaji wa huduma miongoni mwa taasisi za umma (Government to Government), kati ya taasisi za umma na wananchi (Government to Citizens), kati ya taasisi za umma na sekta ya Biashara (Government to Business), na kwa Serikali kuwahudumia watumishi (Government to Employees).

Katika kuendeleza utekelezaji huo, Januari 30 hadi Februari 2, 2019 Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) iliyo chini ya Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliandaa Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao kilichofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Sayansi ya Kompyuta, Habari na Mawasiliano kilichopo Chuo Kikuu cha Dodoma na kuhudhuriwa na washiriki 786 kutoka taasisi za umma wakiwemo Makatibu Wakuu, Maofisa Masuuli wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Wakurugenzi wa TEHAMA, Maofisa TEHAMA na Watumiaji wa mifumo ya TEHAMA Serikalini.

Mtendaji Mkuu wa Wakala hiyo Dkt. Jabiri Bakari anasema lengo la Kikao Kazi hicho ni kubadilishana uzoefu, kuongeza ushirikiano, kujenga uwezo, kuongeza uelewa wa pamoja, kuainisha na kutatua changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini ili kuhakikisha kuwa matumizi sahihi ya TEHAMA Serikalini yanakuwa na tija kwa kuongeza ufanisi, uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi kwa viwango na ubora unaotakiwa.



***Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) Dkt. Jabiri Kuwe Bakari akisisitiza jambo wakati wa Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mandao 2019 UDOM-CIVE***

Akizungumza wakati wa Ufunguzi wa Kikao Kazi hicho kwa Makatibu Wakuu na Maofisa Masuuli wa Serikali Kuu na

Serikali za Mitaa, Naibu Waziri Ofisi ya Rais -Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Mary Mwanjelwa anasema kuwa utekelezaji wa juhudi za Serikali Mtandao umechangia kwa kiasi kikubwa katika kurahisisha utoaji wa taarifa na huduma kwa wananchi kwa haraka, uwazi, urahisi, gharama nafuu, zinazopatikana wakati wowote na mahali popote nchini, na duniani kote.

Dkt. Mwanjelwa anasema kuwa, Serikali imeweka msukumo mpya katika kutekeleza Serikali Mtandao kwa kusisitiza ushirikiano na matumizi ya pamoja ya rasilimali za TEHAMA miongoni mwa taasisi za umma, kutoa miongozo na viwango mbalimbali vya kufuatwa katika utekelezaji wa Serikali Mtandao. Pia, Serikali imedhamiria kuimarisha miundombinu ya TEHAMA, uratibu wa shughuli za TEHAMA na usalama wa taarifa za Serikali ili kuongeza ufanisi katika Sekta ya Umma, kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali na kupanua wigo wa upatikanaji na ubora wa huduma kwa wananchi.



***Naibu Waziri Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Dkt. Marry Mwanjelwa (Mb) akizungumza wakati wa Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019 kilichofanyika UDOM-CIVE***

Dkt. Mwanjelwa anasema tatizo la usalama mitandaoni linazidi kukua kadri maendeleo ya Teknolojia yanavyozidi kukua, hivyo ili kuweza kukabiliana na changamoto hiyo ni lazima taasisi za umma kuzingatia viwango vyote vya usalama kwenye mifumo husika katika utekelezaji wa Serikali Mtandao wakati wa kubuni, kusanifu, kujenga, kusanikisha na kuendesha mifumo ya TEHAMA, badala ya kujenga mfumo kwanza na unapokamilika ndipo masuala ya usalama wa mifumo ya TEHAMA yanafikiriwa. Pia, kutumia na kuzingatia programu ambazo watalaam wetu wanaweza wakatambua kinachofanyika badala ya kuwa na mifumo ambayo hatujui kinachoendelea nyuma ya pazia.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Idara ya Ushauri na Uchambuzi Kazi Bw. Mick Kiliba anasema kuwa iwapo mifumo na miundombinu ya TEHAMA itakuwa imewianishwa na kuwezesha kubadilishana taarifa, itasaidia uboreshajii wa shughuli mbalimbali katika Utumishi wa Umma. Hivyo, taasisi za umma zinatakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao iliyowekwa ili kuboresha utendaji wa Serikali utakao rahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi na hivyo kutuwezesha kuufikia uchumi wa viwanda tunaoutarajia.

Bw. Kiliba anaeleza kuwa, lengo kuu la utekelezaji wa Serikali Mtandao ni kuboresha utoaji wa huduma kwa umma, lakini pia utekelezaji wake unalenga kuimarisha utawala bora na kuongeza tija na ufanisi katika uendeshaji wa taasisi za Umma kwa kuhakikisha kuwapo na mawasiliano ya haraka, yenye uhakika na salama ndani na kati ya taasisi mbalimbali za Serikali; kuanzia kwenye Wizara, Mikoa hadi ngazi za Halmashauri pamoja na taasisi za umma zinazojitegemea na Balozi zetu nje ya nchi.

Aidha, anasema Serikali Mtandao inadhamiria kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali; kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa muhimu katika kila ngazi Serikalini; kuimarisha usalama wa taarifa za Serikali na kuongeza uwezo wa Serikali kupambana na majanga kwa kutumia teknolojia; kurahisisha michakato ya utendaji kazi katika taasisi za Serikali, kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuongeza udhibiti wa mapato ya Serikali.

Akizungumzia suala la usalama wa mifumo ya TEHAMA Serikalini, Mkurugenzi wa Udhibiti wa Huduma za TEHAMA wa Wakala ya Serikali Mandao Bw. Michael Moshiro anasema usalama wa mitandao upo kila mahali kwa sababu hakuna mfumo wowote duniani ambao upo salama kwa asilimia mia moja na Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo.

"Kama Serikali kwa kweli tumejipanga. Kwanza kwenye usalama kuna vitu vitatu na kitu cha kwanza ambacho ni kikubwa kabisa ni watu wakiwemo watumiaji na wataalam. Kwa hiyo katika eneo hilo, Serikali tunaendelea kutoa uelewa wa mambo ya masuala ya mifumo kwa watumishi wetu lakini pia tumeendelea kujenga uwezo wa watumishi wetu ili kulinda na kuikagua mifumo yetu, kujua hatari zilizopo na kuzifanyia kazi. Kwa hiyo tumeweka mifumo na vifaa mbalimbali vinavyoangalia hatari", anafafanua Bw. Moshiro.

Aidha, anasema katika upande wa Teknolojia ambao unaonekana kutishia usalama wa mifumo, Serikali inaendela kujiimarisha kwa kuwa na teknolojia za kisasa zinazosaidia kulinda mifumo na mikakati mbalimbali imetengenezwa ikiwa ni pamoja na mkakati wa kitaifa wa kulinda usalama (National Cybe Security Strategy) na Mkakati wa usalama wa uhalifu wa kimtandao na Mpango Kazi (Government Cyber Security Strategy and Action Plan).

Bw. Moshiro anasema katika mifumo ambayo inabeba utendaji kazi wa Serikali (critical systems), Serikali inahakikisha kuwa mifumo inatengenezwa na wataalamu wa ndani ili kuweza kuona kila kinachoendelea ndani ya mfumo, kuilinda na hata likitokea tatizo kwenye mfumo linashughulikiwa na wataalamu wa ndani.

Naye Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao Dkt. Jabiri Bakari anasema dunia inabadilika kwa kasi kutoka katika mfumo wa viwanda asilia vilivyotokana na mapinduzi ya viwanda ya Karne ya 18 kuelekea katika matumizi makubwa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo yana mchango mkubwa katika kufikia Maendeleo ya Uchumi wa kati unaochochewa na Viwanda ambao ni muhimu.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Huduma za TEHAMA kutoka Wakala ya Serikali Mtandao Bw. Benedict Ndomba anasema kikao kazi hicho kimeleta uelewa wa pamoja wa hali ya matumizi ya TEHAMA katika taasisi za umma, kimesaidia kuweka mkakati wa pamoja wa namna ya kuzitatua changamoto za TEHAMA na kuona jinsi TEHAMA inavyoweza kutumika katika kuijenga Tanzania ya viwanda.

Pia, kimeweka vipaumbele vya kazi mbalimbali za kufanya ambazo zitaboresha matumizi ya TEHAMA Serikalini na hivyo kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma kwa umma, kukubaliana kwa pamoja kwamba taasisi zote za umma lazima zitumie miundombinu na mifumo shirikishi ili kupunguza gharama za matumizi ya TEHAMA katika taasisi za

umma na pia kuweka msisitizo katika matumizi ya tafiti na ubunifu katika Serikali Mtandao ili kuboresha matumizi ya TEHAMA katika kuongeza na kuboresha huduma kwa umma

Kabla ya kuanzishwa kwa Wakala ya Serikali Mtandao, baadhi ya taasisi za Serikali zilikuwa zikitengeneza mifumo ambayo wakati mwingine inafanana kazi na matumizi yake na pia wakandarasi walikuwa wakitumika katika kila hatua ya kutengeneza mifumo, jambo ambalo lilikuwa likitishia usalama a mifumo.

Ili kukabiliana na jambo hilo,Dkt. Bakari anasema Serikali imewajengea uwezo na itaendelea kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA kuhakikisha kuwa mifumo inatengenezwa na kudhibitiwa na wataalam hao na mifumo hiyo inatakiwa kuzingatia miongozo na viwango vya Serikali Mtandao vinavyowekwa na Serikali.

Naye Mkurugenzi wa TEHAMA kutoka Ofisi ya Rais Utumishi Bw. Priscus Kiwango anasema "Jitihada nyingi zimefanyika, tulianza kutoa maelekezo katika taasisi za Serikali kwamba mifumo wanayoiweka iweze kubadilishana taarifa. Tulitoa miongozo na viwango vya Serikali Mtandao ambazo zilisambazwa katika taasisi zote za Serikali ili kila zinapotaka kutekeleza mifumo ya Serikali Mtandao ziweze kuzingatia viwango na miongozo hiyo".

Dkt. Bakari anasema kuwa, Serikali inafanya juhudi kubwa ili kuifanya mifumo iweze kubadilishana taarifa "Kama mifumo haitowasiliana, hakuna Serikali Mtandao, lazima mifumo ifanye kazi sawasawa na lazima iwasiliane ili iwe inasababisha kuongeza ufanisi, kupunguza gharama za utendaji ndani ya taasisi na kuhakikisha kuwa huduma inapotoka kwenda kwa mwananchi kupitia TEHAMA inakuwa ni ya haraka".

Suala la kuunganisha taasisi za umma kwenye mtandao mmoja wa mawasiliano nalo lilishika hatamu na katika hilo, Dkt. Bakari anasema hapo awali taasisi za serikali zilikuwa hazijaungwa pamoja kwa hiyo zilikuwa zikipata mtandao kutoka kwa watoa huduma mbalimbali. Kwa sasa jitihada zimefanyika na taasisi zimeunganishwa pamoja kwenye mtandao wa Serikali (Government Network), kwa hiyo zinaweza kuwasiliana kwa haraka na kwa gharama nafuu ikilinganishwa na hapo awali ambapo kila taasisi ilikuwa imeungwa kwenye mtandao wa kimataifa kwa hiyo zikitaka kuwasiliana lazima zipitie kwenye mtandao huo.



***Baadhi ya washiriki wa Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao wakifuatilia Kikao Kazi hicho.***

Vilevile anasema kuwa, kikao kazi hicho kimekuwa na manufaa makubwa kwa Wakala hiyo kwa kuwa wamepata mirejesho kutoka kwa wadau kuhusu masuala ya Serikali Mtandao ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto za matumizi ya TEHAMA katika taasisi za umma jambo ambalo linatoa fursa ya kuona ni namna gani ya kufanya ili kuweza kuzitatua changamoto hizo kwa kufanya nao kazi kwa ukaribu kwa kuwa Idara zote za TEHAMA ni kitu kimoja na

pia wanapata maarifa ya kutosha ya jinsi gani ya kutumia TEHAMA ili kuboresha utendaji kazi wa taasisi na utoaji huduma kwa umma.

Naye Mkurugenzi wa Usimamizi wa Huduma za TEHAMA Bw. Benedict Ndomba anasema kuna mwamko mkubwa sana wa taasisi za Serikali kushirikiana na kufanya jambo ambalo lina faida na manufaa makubwa kwa nchi kama vile utengenezaji wa Mfumo wa Ukusanyaji Mapato Kielekroni ***-GePG*** uliohusisha taasisi zaidi ya mbili kutengeneza na kwa sasa umekuwa na manufaaa makubwa kwa Serikali na nchi kwa jumla.

"Ni vema taasisi zikashirikiana kutengeneza kitu kimoja chenye faida kwa nchi kuliko taasisi moja kutengeneza mfumo peke yake na hatimaye hakuna taasisi inayomaliza na kujikuta tumepoteza muda na fedha za Serikali, Hivyo nasisitiza kwamba kadiri tunavyoenda mbele ushirikiano na kuweka uzalendo mbele ni muhimu sana ili kuweka wote pamoja na kutumia rasilimali zilizopo kutengeneza kitu kikubwa kuliko kila mmoja akifanya peke yake kwenye taasisi yake', anasema Bw. Ndomba.

Akizungumza wakati wa siku ya Utafiti na Ubinifu wa Serikai Mtandao, Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Maendeleo kwa Wote (UCSAF) Mhandisi Peter Ulanga anasema Dunia inapitia kwenye mapinduzi makubwa sana ya uchumi wa nne wa viwanda unaoleta maendeleo makubwa katika Nyanja ya utoaji huduma na utengenezaji bidhaa ambao utahusisha TEHAMA na mbinu nyingine za utengenezaji, hivyo watumishi wa umma hawana budi kuchangia katika maendeleo yatakayotokea katika uchumi wa nne wa viwanda na njia pekee ya kufanikisha hayo ni kwa kuhakikisha wanatumia vema tafiti na ubunifu wa Serikali Mtandao.

Naye Afisa TEHAMA mwandamizi kutoka Chuo cha Maji (WDMI) Bw. Juma Mchiro anasema Kikao Kazi hicho kimekuwa na tija kubwa kwa kuwa ni sehemu pekee ambayo wataalam wa TEHAMA Serikalini wanakutana na kuzungumzia masuala mbalimbai ya TEHAMA na kuona jinsi gani wanaweza kutumia TEHAMA ili kuweza kurahisisha utendaji kazi na utoaji huduma kwa umma.

Afisa TEHAMA mwandamizi kutoka RITA Bi. Robby Otaigo anasema Miongozo na Viwango vinavyotolewa na Serikali Mtandao ikifuatwa vyema inaleta tija na kwa jumla TEHAMA ikitumika vizuri inasaidia utoaji huduma kwa wananchi hata wa hali ya chini.

Naye Meneja wa Kanda kutoka NMB Bw. Nsolo Mlozi anasema wananchi waendelee kutumia TEHAMA kwa sababu si kitu cha kuchagua tena bali dunia ya sasa ni ya teknolojia na pia ni fursa ambayo inaweza kuhudumia wananchi kwa haraka zaidi.

Naye Afisa Uhusiano Mwandamizi kutoka Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Bw. Sebera Fulgence anasema watumiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano waitumie inavyopasa kwa sababu masuala ya TEHAMA yanaenda kwa kasi zaidi na kwa yeyote anayeitumia vile inavyotakikana basi atayaona manufaa yake.

Kikao Kazi kiliongozwa na Kaulimbiu ya "Uwianishaji wa Rasilimali za TEHAMA kwa Maendeleo ya Viwanda" (Harmonization of ICT Resources for Industrial Development) ambayo

iliandaliwa mahususi kwa ajili ya kuonesha umuhimu wa kutumia rasilimali za TEHAMA kwa ukamilifu na kuhakikisha taasisi za umma zinashirikiana na kutumia mifumo ya pamoja, miongozo na viwango vilivyowekwa ili kuleta maendeleo ya viwanda nchini.



***Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) Dkt. Jabiri Kuwe Bakari akitoa cheti cha ushiriki kwa mmoja wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha St. Joseph wakati wa Siku ya Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao Februari 2, 2019 UDOM-CIVE***

Ni ukweli usiopingika kwamba dunia inaelekea kwenye teknolojia na ili kufikia uchumi wa kati wa maendeleo ya viwanda, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni kiungo muhimu sana kufanikisha hilo. Pia, suala la matumizi ya TEHAMA hayawezi kuepukika kwa kuwa ndio msingi mkuu na inachagiza maendeleo ya sekta mbalimbali kama vile kilimo, Madini, Utalii, Elimu, Afya, Fedha, nk.

Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi Serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi, kupunguza gharama za utendaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Serikali Mtandao siyo teknolojia kama inavyochukuliwa na wengi, bali ni matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utendaji kazi wa kila siku.

**(Mambwana Jumbe ni Ofisa Habari, Eimu na Mawasiliano wa Wakala ya Serikali Mtandao)**